HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA
KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA KWANZA (OKTOBA – DISEMBA, 2023) ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA LEWIS KALINJUNA
TAREHE 15-16. 02.2023

A. WAJUMBE

WALIOHUDHURIA:

1.	Mhe. Elias R. Masumbuko	Mstahiki Meya (Mwenyekiti)
2.	Mwl Alexius R. Kagunze	Mkurugenzi wa Manispaa (Katibu)
3.	Mhe. Zamda S. Mwebea	Naibu Meya
4.	Mhe. James M. Matinde	Mjumbe
5.	Mhe. John P. Kisandu	Mjumbe
6.	Mhe. Picca N. Chogero	Mjumbe
7.	Mhe. Sheilla D. Mshandete	Mjumbe
8.	Mhe. Victor T. Mmanywa	Mjumbe
9.	Mhe. Enock C. Lyeta	Mjumbe
10.	Mhe. Moshi H. Kanji	Mjumbe
11.	Mhe. Hassan R. Mwendapole	Mjumbe
12.	Mhe. Msabila M. Kulwa	Mjumbe
13.	Mhe. Zuhura Waziri	Mjumbe
14.	Mhe. Juma M. Nkwabi	Mjumbe
15.	Mhe. Reuben N. Kitinya	Mjumbe
16.	Mhe. Mussa E. Andrea	Mjumbe
17.	Mhe. Mariam L. Nyangaka	Mjumbe
18.	Mhe. Paschazia C. Seni	Mjumbe
19.	Mhe. Peter J. Kwoliba	Mjumbe
20.	Mhe. Victor Y. Mkwizu	Mjumbe
21.	Mhe. Esther F. Makune	Mjumbe
22.	Mhe. Ezekiel J Sabo	Mjumbe
23.	Mhe. Reuben M. Dotto	Mjumbe
24.	Mhe. Gulamhafeez Mukadam	Mjumbe

B. WASIOHUDHURIA

1.	Mhe. Patrobas Katambi (MB)	Kwa taarifa
2.	Mhe. Lucy Mayenga (Mbunge VM)	Kwa taarifa

C. WATAALAM

1. Pius M. Sayayi	Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu.
2. Kuchibanda K. Snatus	Mkuu wa Kitengo cha usimamizi wa Taka na Usafi wa Mazingira.
3. Charles Luchagula	Mkuu wa Kitengo cha Utamaduni, Michezo na Vijana
4. Jesca Kipingu	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.
5. Mensaria Mrema	Mkuu wa Divisheni ya Mipango na uratibu
6. Naely Elias	Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji
7. Lenard Chepe	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA.
8. Eng Boaz Kayira	Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu, maendeleo ya Vijiji na Miji.
9. Peter Chuwa	Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani.
10. John Tesha	Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii.
11. Ezra Manjerenga	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhifadhi wa Maliasili na Mazingira.
12. Mary S. Maka	Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi
13. Lucas Mzungu	Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari.
14. Octavina Kiwone	Mratibu TASAF
15. Jacob Mwinuka	Afisa Ardhi Mteule wa Ofisi ya Ardhi Manispaa.
16. Simon Shoo	Kny ya Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi
17. Dr Elisha Robert	Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe.
18. Richard Massawe	Mthibiti Ubora wa Shule.
19. Consolata James	Kny ya Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi
20. CPA Kishenyi Mulokozi	Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu
21. Rose Matunda	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria.
22. CPA Sunday Nkwambi	Mhasibu wa Mapato

D. WAALIKWA

1. Ibrahim M. Makana	-	Kny RAS
2. Said R. Kitinya	-	DAS
3. Violet Lumelezi	-	Kny AAS-MMI
4. Evarst Kivuyo	-	Kny OCD
5. LT Col Ford J. Mwakasege	-	MJA
6. Santus J. Mang'ee	-	Kny DBC
7. Martin Kunambi	-	SSP- Mkuu wa Gereza
8. Fredy Hadson	-	Kny DSO
9. S/SGT Masoud M. Mwagilo	-	Kny DFO
10. Anold Makombe	-	M/Kiti CCM (W)

11. Ally Shabani - Katibu CCM (W)
12. Samwel Jackson - Katibu wa Mbunge

E. WAKUU WA TAASISI

1. Eng Daniel Ojwando - TEMESA
2. Nkinda Senni - RUWASA
3. Eng. Ibrahim Kiyungu - TANESCO
4. Eng Yohana William - TARURA
5. Eng Uswege Musa - SHUWASA

F. WATENDAJI WA KATA

1. Gaudiozi K. Mwombeki - Mtendaji wa Kata ya Ngokolo
2. Fortunatus L. Jilala - Mtendaji Kata ya Chamaguha
3. Elizabeth S. Mbate - Kny Mtendaji wa Kata ya Kolandoto
4. Adella Mukinga - Mtendaji wa Kata ya Kizumbi
5. Joshua Masengwa - Mtendaji wa Kata ya Ndala
6. Mwakaluba Jacob - Mtendaji wa Kata ya Old Shinyanga
7. Costantine M. Masalu - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Masekelo
8. Mahiba Pastory - Mtendaji wa Kata ya Lubaga
9. Abdul Kumalija - Mtendaji wa Kata ya Mwawaza
10. Simon Mashishanga - Mtendaji wa Kata ya Mjini
11. Patrick M. Dotto - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Ibinzamata
12. Mayala Ibrahim - Mtendaji wa Kata ya Kitangili
13. Michael Joshua - Mtendaji wa Kata ya Mwamalili
14. Sarah Wankuru - Mtendaji wa Kata ya Kambarage
15. Emilini Mtambu - Mtendaji wa Kata ya Ndembezi
16. Antony Charles - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Ibadakuli
17. Ponsian Ngodita - Mtendaji wa Kata ya Chibe

F: AFISA TARAFA

1. Aaron L. Laizer - Kaimu Afisa Tarafa ya Mjini
2. Gregory Kachira - Afisa Tarafa ya Ibadakuli
3. Neema Mukandala - Afisa Tarafa ya Old Shinyanga

G: WAANDISHI WA HABARI.

1. Ibrahim Rojala - Jambo Fm
2. Amos John - Kwizera
3. Kadama Malunde - Mwandishi
4. Stela Ibengwe - Mwandishi
5. Mwamvita Issa - Mwandishi
6. Arnold Rukiza - SHY-MC

SEKRETARIETI

1. Macelina Bwathondi — Mwandishi wa Vikao
2. Esther Daudi — Mwandishi wa Vikao
3. Amina Juma — Mwandishi Mwendesha Ofisi

Agenda za kikao zitakuwa kama ifuatavyo: -

Siku ya kwanza tarehe 15.02.2024

1. Kufungua mkutano
2. Kuthibitisha agenda za mkutano.
3. Kupokea na kujadili taarifa za kwenye Kata kutoka kwa Madiwani wa Kata husika Pamoja na majibu ya changamoto za Kata kwa kipindi cha robo ya kwanza.
4. Kuahirisha kikao

Siku ya pili tarehe 16.02.2024

5. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani wa kawaida wa tarehe 30- 31.10.2023.
6. Kupokea Mihtasari ya Kamati za Kudumu kwa robo ya kwanza ya mwaka 2023/2024
   - Kamati ya Kudhibiti UKIMWI tarehe 13.10.2023
   - Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu wa tarehe 17.10.2023.
   - Kamati ya Mipango Miji na Mazingira wa tarehe 18.10.2023.
   - Kamati ya Fedha na Utawala wa tarehe 20.10.2023, 29.11.2023 na 19.12.2023.

7. Kupokea taarifa za utekelezaji wa Idara mbalimbali za kamati za kudumu kwa robo ya pili 2023/2024.
   - Kamati ya kudhibiti UKIMWI
   - Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu
   - Kamati ya Mipangomiji na Mazingira
   - Kamati ya Fedha na Utawala
8. Taarifa kutoka kwa Mkurugenzi kama zipo.
9. Masuala ya kiutumishi.
10. Kufunga kikao.

AGD Na.01:2023/24 **MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

Kumb: BAR.02.1.1 Mkutano wa Baraza la Madiwani wa kupitia taarifa ya robo ya pili 2023/2024 Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe kuuliza maswali ya papo kwa papo kama ifuatavyo;

Kumb: BAR.02.2.2 **Swali:** Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ina mpango gani wa kuendeleza Machinjio ya zamani.

Jibu: Ufafanuzi ulitolewa kuwa machinjio ya zamani iliacha kutumika baada ya kufunguliwa machinjio ya Kisasa ya Ndembezi. Katika Bajeti ya mwaka 2024/2025 Machinjio ya zamani itafanyiwa ukarabati na itatumika kama machinjio ya Kuku.

Kumb: BAR.02.2.3

Swali: Ni lini Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga itakamilisha Stendi ya Kambarage kwenda Old Shinyanga.

Jibu: Ufafanuzi ulitolewa kuwa Stendi ya Kambarage ilishakamilika kwa robo ya tatu 2023/2024 itaanza kufanya kazi. matengenezo yamekamilika ya kibanda cha kupumzikia Abiria na choo cha kuanzia kazi. Ilielezwa kuwa kulikuwa na mpango wa kutoa mkopo kwa vikundi kwa ajili ya kununua Daladala (Hiace) kwa ajili ya kutoa huduma ya usafiri kwa wakazi wa Kata zote za Shinyanga Manispaa.

Kumb: BAR.02.2.4

Swali: Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ina mkakati gani wa kukaa na RUWASA, SHUWASA ili kupeleka maji kwenye Kijiji cha Bushola kwakuwa kuna mradi wa maji unaopita hapo kuelekea Wilaya ya Kishapu?

Jibu: Ufafanuzi ulitolewa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga itakaa na RUWASA, SHUWASA na KASHWASA kuona umuhimu wa kupitisha maji katika Kijiji cha Bushola ili kuondoa tatizo la uhaba wa maji kwa wakazi hao.

Kumb: BAR.02.2.5

Swali: Kutokana na kero ya ndege kwenye mtaa wa majengo karibu na eneo la Maziko ambao ndege hao wanatoa manyonya madogo madogo na kinyesi kinachochafua mazingira yanayosumbua wakazi wa eneo hilo, ni lini Halmashauri itawaondoa ndege hao?

Jibu: Ufafanuzi ulitolewa kuwa kulikuwa na jitihada kupata kibali kutoka BAKWATA ili kuingia eneo la maziko (Makaburini) ili kuwaondoa ndege hao waharibifu. Wito ulitolewa kwa wakazi wa maeneo hayo kufanya usafi wa mazingira kwakuwa ndege hao wamekuwa wakivutiwa na mazingira yenye matope na takataka nyingi. Jitahada za kuwaondoa ndege waharibifu zinaendelea kwa kuanza kuwatafutia makazi ili kuwahamisha. Aidha kibali cha BAKWATA kikitoka yatasafishwa mazingira hayo ya maziko kwa kukata matawi katika maeneo hayo ili ndege hao wahame katika maeneo hayo.

Kumb: BAR.02.2.6 **Swali:** Ni lini Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga itakamilisha ujenzi wa kituo cha Polisi kilichopo Kata ya Ngokolo katika Soko la Majengo Mapya ambacho kituo hicho kilijengwa kwa nguvu za Wananchi.

Jibu: Ufafanuzi ulitolewa kuwa katika uandaaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 itaangaliwa kama kuna sehemu utawekwa mpango wa ukamilishaji wa kituo hicho cha polisi.

AGD Na.01:2023/24 **KUFUNGUA MKUTANO**

Kumb: BAR.02.3.1 Mwenyekiti alifungua Mkutano wa Baraza la Madiwani robo ya pili saa 05.40 asubuhi kwa kuwakaribisha Wajumbe, Kamati ya ulinzi, Waandishi wa Habari na Wananchi katika Mkutano wa Baraza la Madiwani.

AGD Na.02: 2023/24 **KUTHIBITISHA AGENDA ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 15 - 16 .02. 2024.**

Kumb: BAR .02.4.1 Jumla ya agenda 10 zilithibitishwa kwenye Mkutano wa kawaida wa wa Baraza la Madiwani.

AGD Na.03 :2023/24: **KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA KWENYE KATA KUTOKA KWA MADIWANI WA KATA HUSIKA.**

Kumb: BAR.02.5.1 Wajumbe waliwasilisha taarifa na changamoto za kila Kata husika na walionesha utatuzi wa Changamoto hizo, Wajumbe waliipongeza Menejimenti ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kwa jitihada zilizofanyika za kutatua changamoto katika Kata, hivyo kupelekea maswali kupungua. Aidha waliendelea kutoa wito kwa Menejimenti kuendelea kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani katika kupunguza changamoto ili kuleta Maendeleo katika Manispaa.

Kumb: BAR.02.5.2 Aidha Wajumbe walihitimisha taarifa za utekelezaji wa Kata kwa kuweka msisitizo katika kuzingatia suala la usafi hasa katika usafi wa masoko. Walieleza kuwa Wafanyabiashara waendelee kukumbushwa kuzingatia usafi katika maeneo wanayofanyia kazi.

AGD Na.04 :2023/24: **KUAHIRISHA KIKAO**

Kumb: BAR.02.6.1 Kikao cha kujadili taarifa za Kata kiliahirishwa saa 6:40 mchana

SIKU 2 **16.02.2024**

AGD Na.06:2023/24: **KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 30-31.10.2023.**

Kumb: BAR.02.7.1 Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe 30-31.10.2023. ulisomwa ukurasa kwa ukurasa na wajumbe kuridhia kuwa yaliyomo ndiyo yaliyojadiliwa na hivyo ulithibitishwa na kuwa kumbukumbu halali wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kwa Mwenyekiti na Katibu kusaini Muhtasari huo.

AGD Na.06:2023/24: **KUPOKEA MIHTASARI YA KAMATI ZA KUDUMU YA ROBO YA KWANZA 2023/2024.**

Kumb: BAR.02.8.1 Kupokea Mihtasari ya Kamati za Kudumu kwa robo ya kwanza ya mwaka 2023/2024 ambayo tayari ilishathibitishwa katika vikao vya Kamati vilivyofanyika;

- Kamati ya Kudhibiti UKIMWI wa tarehe 13.10.2023
- Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu wa tarehe 17.10.2023.
- Kamati ya Mipango Miji na Mazingira wa tarehe 18.10.2023.
- Kamati ya Fedha na Utawala wa tarehe 20.10.2023, 29.11.2023 na 19.12.2023.

Kumb: BAR.02.8. 2 Wajumbe waliipokea Mihtasari ya Kamati za kudumu na kuridhia kuwa kumbukumbu halali ya vikao vya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

AGD Na.07:2023/24: **KUPOKEA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA IDARA MBALIMBALI ZA KAMATI ZA KUDUMU KWA ROBO YA PILI 2023/2024**.

Kumb: BAR.02.9.1 Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Divisheni na Vitengo mbalimbali vilivyo chini ya Kamati za Kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ambazo ni Kamati ya Uchumi Afya na Elimu, Kamati ya Mipango Miji na Mazingira, Kamati ya Kudhibiti UKIMWI, Kamati ya Fedha na Utawala kwa robo ya kwanza 2023/2024 iliwasilishwa kwa Wajumbe. Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili.

Kumb: BAR.02.9.2 **Wajumbe walitoa hoja kuwa itengwe siku kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani kuhusiana na mfumo wa TAUSI ili kuufahamu mfumo, changamoto zake na jinsi unavyofanya kazi.**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa mafunzo ya Waheshimiwa Madiwani kuhusiana na mfumo wa TAUSi yatafanyika katika mpango na Bajeti wa 2024/2025.

Kumb: BAR.02.9.3 Wajumbe walitoa hoja kuwa kutokana na changamoto za kimfumo hasa utoaji wa namba za malipo (Control Number), Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga iombe kibali kutoka TAMISEMI cha kupokea fedha nje ya mfumo kwa kutumia risiti za kawaida ili mfumo utakapotengemaa fedha hizo ziweze kuwekwa Benki kuliko kupoteza mapato hayo.

Ufafanuzi ulitolewa na Kaimu RAS kuwa mfumo wa TAUSI uko vizuri na umeondoa changamoto nyingi na kurahisishwa kwa Watumiaji isipokuwa tatizo linalojitokeza la Mtuamiaji mmoja mmoja. Aidha Wafanyabiashara waendelee kupewa elimu kuhusiana na matumizi sahihi ya mfumo wa TAUSI ili kuleta tija katika ukusanyaji wa mapato. Ilifafanuliwa zaidi kuwa panapotokea changamoto za kimfumo taarifa itolewe kwa Afisa TEHAMA katika ngazi ya Mkoa ili kuzifanyia kazi kwa haraka zaidi.

Kumb: BAR.02.9.3 Aidha Wajumbe waliipongeza timu ya Menejimenti hasa Kitengo cha huduma za Sheria kwa usimamizi mzuri wa kesi zote na hivyo kupelekea kesi nyingi za Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kushinda**.**

AGD Na.08:2023/24: **TAARIFA KUTOKA KWA MKURUGENZI.**

Kumb: BAR.02.10.1 **TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO ZA MWAKA 2023/2024 KWA KIPINDI CHA ROBO III KIASI CHA TSH 1,131,000,586**

Kumb: F/A 02.10.2 Taarifa iliwasilishwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga mnamo tarehe 10.01.2024 ilipokea kiasi cha Sh 1,131,000,586.00 kwa Exchequer EB/AG/159/23/3961 kwa ajili ya maandalizi ya kupokea kidato cha kwanza 2024. Fedha za miradi hii zilipokelewa nje ya bajeti ili kujenga miundombinu kwa Shule za Sekondari 11. Miundombinu hiyo ni matundu ya vyoo 80 kiasi cha Sh 144,000,000, vyumba vya madarasa 27 kiasi cha Sh 702, 000, 000 na ukamilishaji wa bwalo la chakula kiasi cha Sh 285,000,586.

Kumb: BAR.02.10.3 Wajumbe waliipokea taarifa na kutoa salaam zao za pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa awamu ya Sita Dr. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta fedha za Maendeleo za ujenzi wa miundombinu katika Shule za Sekondari.

Kumb: BAR.02.10.4 **TAARIFA YA UFAFANUZI WA KUSITISHWA UTOAJI MIKOPO ITOKANAYO NA ASILIMIA 10 YA MAPATO YA NDANI.**

Taarifa Iliwasilishwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ilipokea barua kutoka kwa Katibu Tawala Mkoa ya tarehe 21.04.2023 ambayo ilielekeza kusitishwa mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani.

Kumb: BAR.02.10.5 **Ilielezwa kuwa** barua hiyo ilitokana na maelekezo yaliyotolewa Mkoani kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, kufuatia maelekezo ya Mhe Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kutokana na maelekezo hayo barua iliyowasilishwa ilielekeza kufanya yafuatayo;

- Kusitisha utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu.
- Kuendelea kutenga na kupeleka fedha hizo kwenye akaunti maalum kwa mujibu wa kifungu cha 37 A cha Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kama zilivyotengwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha husika.
- Kuhakikisha Halmashauri inaongeza nguvu katika kufuatilia marejesho ya fedha zote zilizokopeshwa kulingana na mikataba kati ya Halmashauri na vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu.

Wajumbe waliipokea taarifa na kuipitisha**.**

Kumb: BAR.02.10.6 **TARURA**

Taarifa iliwasilishwa kuwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA) Manispaa ya Shinyanga ina Mtandao wa Barabara wenye urefu wa Km 780.184, kilometa 193.6345 ni Barabara zinazounganisha Kata na zinazounganisha Tarafa na Wilaya jirani (collector Roads)

Kilometa 586.549 ni Barabara zinazounganisha Kata na Vijiji (feeder Roads). Aidha Halmashauri ina mtandao wa km 22.562 za lami, kilometa 193.156 za changarawe na kilometa 564.466 za udongo.

Kumb: BAR.02.10.7 Kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 TARURA Manispaa ya Shinyanga ilitengewa Sh 2,932,810,000.00 katika fedha hizi, fedha za matengenezo ya Barabara ni Sh 1,432,810,000.00 fedha za jimbo ni Sh 500,000,000.00 na fedha za tozo ya mafuta ni Sh 1,000,000,000.00 Aidha fedha zilizopokelewa ni jumla ya Sh 319,260,882.00 sawa na asilimia 10.9 %.

Kumb: BAR.02.10.8 TARURA Manispaa ya Shinyanga inaendelea na utekelezaji wa miradi ya matengenezo ya Barabara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya mikataba 4 ambayo ni asilimia 33 ya utekelezaji. Miradi hiyo

4 ni ya fedha za mfuko wa Barabara (Road Fund) yenye thamani ya Sh 670,118,253.25 ambayo inatekeleza katika baadhi ya Kata za Manispaa ya Shinyanga. Kwa kipindi hiki miradi hiyo ilifikia 65%.

Aidha kuna miradi 3 ya fedha za mfuko wa Barabara ambazo zipo kwenye mchakato wa manunuzi.

Wajumbe waliipokea taarifa na kuipitisha

Kumb: BAR.02.10.9 **SHUWASA**

Taarifa iliwasilishwa kuwa Mamlaka ya Majisafi na usafi wa Mazingira Shinyanga inandelea na utekelezaji wa mradi wa kuongeza mtandao wa majisafi kwa kutumia fedha za ndani katika eneo la Manispaa ya Shinyanga. Mradi huu wa kuongeza mtandao a majisafi una takribani kilometa 16 katika eneo la huduma la SHUWASA ulikadiriwa kutumia kiasi cha fedha takribani Sh 253,000,000 hadi kukamilika kwake.

Kumb: BAR.02.10.10 Ilielezwa kuwa Hadi kufikia mwishoni mwa robo ya pili ya mwaka wa fedha 2023/2024 kiasi cha fedha Sh 87,380,000 zilitumika katika utekelezaji wa mradi wa kuongeza mtandao katika eneo la Manispaa ya Shinyanga katika maeneo yaliyopo Kata zifuatazo; Kitangili (Iwelyangula), Ibadakuli (Mpera C, TANESCO, Bugweto), Chibe (Mwalugoye), Mwawaza (Negezi), Masekelo (Ishoshandili) na Kolandoto. Utekelezaji wa mradi huu ulifikia asilimia 90 ambapo takribani Kilometa 7.6 za mtandao wa bomba zimelazwa katika eneo la Mnaispaa ya Shinyanga.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa.

AGD Na.09:2023/24: **MASUALA YA KIUTUMISHI**

Kumb: BAR.02.11.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ilipata kibali kwa ajira mpya ambapo iliajiri Watumishi 33, kwa Kada za Afya Watumishi 30 na Utawala 3.

Kumb: BAR.02.11.2 Aidha kwa mujibu wa Kanuni D.40 ya kanuni za kudumu katika Utumishi wa Umma toleo la Mwaka 2009 ikisomwa kwa pamoja na kanuni ya 14 (1-7) ya kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 Mtumishi wa ajira mpya anastahili kuthibitishwa kazini anapotimiza miezi 12 kuanzia tarehe ya ajira.

Kumb: BAR.02.11.3 Wajumbe waliipitia taarifa na kuridhia jumla ya Watumishi 30 wa Kada ya Afya na Watumishi wa Utawala 3 kuthibitishwa kazini.

AGD Na.10:2023/24: **KUFUNGA MKUTANO**

Kumb: BAR.02.12.1 Mwenyekiti alifunga Mkutano saa 8:00 mchana kwa kuwashukuru Wajumbe, waalikwa, Waandishi wa Habari, Wananchi pamoja na Wataalam kwa kushiriki vizuri Mkutano wa Baraza la Madiwani.

KUMBUKUMBU HIZI ZIMETHIBITISHWA NA

_____ _____

Mwl Alexius R. Kagunze Mhe. Elias R. Masumbuko

KATIBU **MWENYEKITI**

TAREHE_____